HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO
SHULE YA SEKONDARI SHITA
S.L.P. 31
MWANGOI- LUSHOTO

Barua Pepe_____
Kumb. Na._____
Jina la Mwanafunzi _____
S.L.P. _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHITA
WILAYA YA LUSHOTO MKOA WA TANGA -2021

Utangulizi

Shule ya sekondari Shita inayo furaha ya kukuarifu kuwa wewe _____ umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika Sekondari ya SHITA iliyopo kata ya Mwangoi wilayani Lushoto.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 Na unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 .kushindwa kuripoti katika muda huo na bila kuwepo kwa taarifa zozote, mwanafunzi atachukuliwa kuwa mtoro na hatua za kinidhamu zitachukuliwa juu yake.

MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

1.0 (a) Sare za Shule hii

KWA WAVULANA

- Suruali ya kijivu na shati jeupe mikono mifupi
- Soksi nyeupe na viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba
- Sweta la rangi ya kijivu mikono mirefu
- Bukta na T-shirt ya rangi ya Njano au Nyekundu

KWA WASICHANA

- Sketi ya kijivu (iwe ndefu na yenye heshima), Shati jeupe mikono mifupi na Nusu kanzu nyeupe.
- Soksi nyeupe na viatu vyeusi vya ngozi na vyenye kamba
- Hijab nyeupe (kwa wanafunzi wa Kiislamu)
- Trak-suti na T-shet ya rangi ya blue.

2.0 MAHITAJI MENGINE

(i) Begi la kubebea daftari, daftari 12 aina ya kaunta book quire two na kuendelea, kamusi ya kiingereza, mkebe na kalamu.
(ii) Ufagio wa chelewa mmoja (1) na ndoo ndogo kwa ajili ya usafi.
(iii) Chakula kwa wanafunzi ni muhimu. (wazazi watatoa utaratibu katika kikao cha wazazi)

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule ya sekondari Shita inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya waziri Mkuu- TAMISEMI yenye Jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
(i) Kutunza mali za Umma.

3.1 **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

(a) Wizi
(B) Uasherati Na Ushoga
(C) Ubakaji
(D) Ulevi Na Matumizi Ya Madawa Ya Kulevya, Kama Vile Uvutaji Wa Bangi, Coceine, Mirungi, Kubeli Na Kadhalika.
(E) Kupigana Na Kupiga
(F) Kuharibu Kwa Makusudi Mali Ya Umma
(G) Kudharau Bendera Ya Taifa
(H) Kuwa Mjamzito/ Kupata Mimba
(I) Kuoa / Kuolewa
(J) Kutoa Mimba
(K) Kugoma, Kuchochea Na Kuongoza Au Kushiriki Kuvuruga Amani Na Usalama Wa Shule Au Watu.
(L) Kukataa Adhabu Kwa Makusudi
(M) Kuwa Na Simu Ya Mkononi (Kumiliki Simu Ya Mkononi)

4.0 **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutokushiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai

(c) Form ya mzazi kuhusu kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHITA SEKONDARI

;

_____

MKUU WA SHULE

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A THE HEADMISTER,

SHITA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 31
LUSHOTO– TANGA.

TO,
The Medical office,
……
……
…….
…….(Name of student in full) please examine the above mentioned student as to her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following category (a- c)

a. (i). Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal disease (v) Limbs

b. Neurosis

c. Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc

Name …… Date ……..signature ……
PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(to be completed by a Government Medical Officer) I have examined the above student and consider that she is fit/unfit full time studies.

i. Eyesight …….

ii. Hearing ……

iii. Speech ……..

iv. Limbs ……

v. Venereal diseases …….

vi. Leprosy …….

vii. Epilepsy ……

viii. Neurosis ……

ix. Other serious diseases eg. Asthma ……..

x. T.B …….

Other Comments ……
Name …….. Date …… Signature ……
STATION …….. DESIGNATION ……..

Official stamp……..